


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI**



TAARIFA KWA UMMA

Maendeleo ya Kuanzishwa kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

Katika kuimarisha usimamizi wa sekta ya maji vijijini, Serikali imeanzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Rural Water Supply and Sanitation Agency-RUWASA). Wakala huyu ameanza kazi rasmi tarehe 01 Julai, 2019 na tayari ameshaanza kazi. RUWASA amekabidhiwa na anaendelea kusimamia jumla ya miradi 652 vijijini ambayo ipo katika wilaya/halmashauri zote nchini.

Katika kipindi cha Mwezi Julai hadi Oktoba, 2019 jumla ya miradi ya maji 69 imekamilika yenye vituo vya kuchotea maji **1549** na ambayo inahudumia watu 412,250. Kwa ujumla kasi ya usimamizi wa miradi imeongezeka tangu kuanza kazi kwa RUWASA ambapo sasa wastani wa maendeleo ya miradi ni asilimia 64 ukilinganisha na asilimia **53** wakati RUWASA inaanza.

Kwa ujumla, katika kipindi cha robo ya kwanza ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2019/2020 jumla ya miradi **108** imelipwa jumla ya shilingi bilioni **14.2**. Miradi hii inatarajiwa kuhudumia wananchi wapatao **1,120,623** katika maeneo ya vijijini.

Ili kuendelea kuimarisha usimamizi wa miradi ya maji vijijini, Wizara ya Maji imefanya mabadiliko ya uongozi wa RUWASA katika mikoa na wilaya. Katika mabadiliko haya tumechukua hatua zifuatazo:

- (i) Tumetengua baadhi ya Mameneja wa Mikoa na Wilaya na kuwapangia vituo vipya vya kazi kama wahandisi wa kawaida.
- (ii) Kuhamisha vituo vya kazi baadhi ya Mameneja wa Mikoa na Wilaya.
- (iii) Kufanya uteuzi wa Mameneja ngazi ya mikoa na wilaya ili kujaza nafasi ya waliotenguliwa.

Mabadiliko haya yameonyeshwa katika jedwali lililoambatishwa.

Prof. Kitila Mkumbo
KATIBU MKUU
Wizara ya Maji